**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**

SHULE YA SEKONDARI LUKOLE,

S.L.P. 41,

**NGARA**.

15/06/2023.

**MAWASILIANO**

| | |
|---|---|
| 0628 185 677 / 0625 198 912 | **MKUU WA SHULE** |
| 0783 230123 / 0765326232 | **MAKAMU MKUU WA SHULE** |
| 0769646939 | **MWALIMU WA FEDHA** |
| 0756279126 | **MATRON** |

Kumb. Na. LUK.SS/UT/06/14 …………………………...

MZAZI WA…… …………………………………………

S.L.P. …………………………………………………..…

…………………..………………………………………

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUKOLE HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA MKOA WA KAGERA MWAKA 2023**

**1.** Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule hii kwa mwaka 2023/2024 tahasusi ya HGL, HGK, HKL, HGE, CBG na EGM. Shule ya sekondari LUKOLE ipo umbali wa Km 18 kutoka mji mkuu wa Wilaya ya Ngara. Kutoka kituo cha mabasi Ngara mjini nauli ni sh 4000/= mpaka shuleni hapa.

**2.** Shule ipo eneo linaloitwa K9 ni karibu sana na barabara. Kwa wanafunzi wanaotokea maeneo ya Mwanza, Bukoba, Karagwe na Kahama washukie katika kituo cha mabasi cha K9 na hapo watakiona kibao cha shule, ni Mita 50 tu kutoka katika kituo hicho.

**3.** Muhula wa Masomo utaanza tarehe **14/08/2023**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023**.

**4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**4.1. SARE YA SHULE**

4.1.1. Sare ya shule hii ni shati mbili (02) nyeupe zenye mikono mirefu (unaweza kuzipata jitrani na shuleni kwa gharama ya Tsh 12,000/=)

4.1.2 Suruali mbili kwa wavulana na sketi mbili kwa wasichana (unaweza kuzipata Jirani na shule kwa gharama ya

- Tsh 18,000 kwa kila suruali moja yenye vipimo vifuatavyo upana kwa chini ni nchi 16 na iwe na mfuko mmoja nyuma, modo **haziruhusiwi kabisa**
- Tsh 18,000 kwa kila sketi moja yenye urefu wa **sentimita 20** kuanzia magotini kwenda chini.

4.1.2.1 Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba kwa wavulana na wasichana. Pia mvulana aje na mkanda wa ngozi mweusi.

4.1.3 Soksi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana ( unaweza kuzipata Jirani na shule kwa gharama ya tsh 3000/= )

4.1.4. Tai (unaweza uipata Jirani na shuleni kwa gharama ya Tsh.5000/= )

4.1.4. Rangi ya hijabu iwe **Nyeupe** kwa wasichana wa kiisilamu watakaopenda kuvaa Hijabu.

4.1.5. Sweta ya rangi ya bluu (Dakar Blue), (unaweza kuipata Jirani na shuleni kwa gharama ya shilingi 15,000/=)

**NB**: ***Maeneo haya yana baridi sana hivyo sweta ni lazima.***

**4.2. SARE BAADA YA MASOMO (SHAMBA DRESS).**

4.2.1. Wavulana wanatakiwa kuwa na suruali mbili.

4.2.2. Wasichana wanatakiwa kuwa na sketi mbili

4.2.3. Sare ya michezo

4.2.4. Rangi ya hijabu baada ya masomo itakuwa yenye rangi ya kijivu kwa waschana wa kiislamu watakao hitaji kuvaa hijabu.

**5. MICHANGO MBALIMBALI:**

5.1.

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Angalizo:** **Jumla ya michango kwa Mwanafunzi ni shilingi 80,000/= (elfu themanini tu) kwa mwaka.**

**Kumbuka**; Ni marufuku kwa mwanafunzi/mzazi/mlezi kuleta fedha za michango mkononi zote zilipwe bank kwenye Account ya shule yenye jina la **LUKOLE SECONDARY SCHOOL CAPITATION GRANT ACCOUNT No. 32101200054** Tawi lolote la **NMB.** Tutapokea risiti ya bank yenye jina la mwanafunzi. Aidha, kwa wale wanaolipiwa na wafadhili wakumbuke kuleta uthibitisho wa maandishi yanayoonyesha aina ya malipo watakayolipiwa.

**6. VIFAA VYA USAFI**

6.1. Ndoo, beseni
6.2. Mifagio ya chepeo miwili.
6.3. Fyekeo
6.4. Rubber squeezer
6.5. Soft broom / Hard broom
6.6. Jembe na mpini wake
6.7. Panga

**Angalizo: vitu vyote ni lazima na vinapatikana shuleni kwa bei ya sokoni.**

***7.*** **VIFAA VYA KULALIA**

7.1. Godoro la 2 ½ x 6 linapatikana shuleni kwa bei ya sokoni
7.2. Shuka 2 za rangi ya pink
7.3. Blanket 1, ni lazima kwa sababu eneo hili kuna baridi

**8. VIFAA VYA CHAKULA**

8.1. Sahani
8.2. Bakuli

8.3. Kijiko

8.4. Kikombe cha ½ lita cha plastiki

**NB. Vifaa vyote vinapatikana kwa bei ya sokoni shuleni**

**9. VIFAA VYA DARASANI**

9.1. Counter book 8 (Quire Three).

9.2. Kalamu za kutosha,

9.3. Mwanafunzi wa HGE/ CBG aje na Tsh 35,000/= kwa ajili ya scientific calculator na mwanafunzi wa mchepo wa EGM aje na Tsh 45,000/= kwa ajili ya scientific calculator. Kwa wanafunzi wote wanaosoma somo la Jiografia waje na mathematical set.

9.4 Dissecting Kit kwa wanafunzi wa CBG. Dissecting Kit zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 35,000/=.

9.5. Wanafunzi wanunue kamusi aina ya **Oxford Advanced Learners Dictionary**. Kwa ambaye hana kamusi hiyo, inapatikana shuleni kwa bei ya sokoni.

**10**. **UJE** na vifaa vyako vya matumizi ya kila siku kama vile taulo, dawa za meno, mswaki, sabuni za kuogea na kufulia, mafuta n.k. Ni vyema pia ukaja na sanduku la mbao au la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyako. **Kumbuka nguo za kiraia ambazo si sare za shule, ambazo hazikutajwa katika fomu hii haziruhusiwi kuvaliwa shuleni**.

**11**. **Ni MARUFUKU** kwa mwanafunzi kuja na simu shuleni pamoja na vifaa vinavyotumia umeme; kama vile radio, chaja, n.k.

**12**. Kila Muhula mwanafunzi aje na rimu 1 ya karatasi (photocopy paper - A4 DOUBLE A) kwa ajili ya majaribio na mitihani.

**13**. Mwanafunzi aje na Tsh 3,000/= kwa ajili ya picha (passport size). Zitapigwa shuleni.

**14**. Kadi ya bima ya afya aina ya NHIF ni ya lazima kwa kila mwanafunzi. Kama mwanafunzi hana kadi hiyo, aje na shilling 50,400/= kwa ajili ya kujiunga na huduma ya NHIF.

**15**. **SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na

Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

***Sheria na Kanuni za Shule***

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

***Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na*:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule:** **0628 185 677**
- **Makamu Mkuu wa Shule:** **0620 102 352**
- **Mwandamizi Taaluma:** **0765 660 114**
- **Mwandamizi Malezi:** **0759 145 446**

**16. MAMBO MENGINE MUHIMU**

16.1. Fomu ya 'Medical examination' imeambatanishwa ijazwe na mganga mkuu wa hospitali ya serikali na ikabidhiwe mara tu mwanafunzi anaporipoti shuleni.

16.2. Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi yaani mkataba wa kutoshiriki katika migomo, kumiliki simu, kufanya fujo na makosa ya jinai. Fomu hii inakipengele cha mzazi kukiri, kukubaliana na sheria, kanuni, michango na maelekezo mengine ya shule.

***Tafadhali soma kwa makini maagizo/maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI LUKOLE**

HEADMASTER
LUKOLE HIGH SCHOOL
Box 41 NGARA

……………………………

JANUARIUS K. RUGAIMUKAMU

**MKUU WA SHULE**

**FOMU HII IJAZWE NA IREJESHWE SHULENI**

Mimi (Jina la Mwanafunzi) …………………………………………………… naahidi kuwa mtiifu wa sheria na kanuni zote za shule. Sitashiriki katika vitendo viovu kwa muda wote nitakao kuwa shuleni kwa mfano: kumiki simu shule, kushiki kwenye migomo, fujo, makosa ya jinai n.k.

Sahihi …………………………………… (Mwanafunzi) Tarehe …………………………

Mimi (Jina la Mzazi/mlezi) ……..…………...……………………………………………….
Mzazi/Mlezi wa …………………………………………………. nakiri kusoma maelekezo na masharti yote ya shule, nakubaliana na sheria, kanuni, taratibu, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Sahihi ………………… (Mzazi/mlezi) Simu ……………… Tarehe …………………...

Namba za simu na picha za wazazi/walezi

(i) Jina ………………………………… No. Simu …………………. Uhusiano ……………

PICHA YA MZAZI/MLEZI TAJWA

(ii) Jina ………………………………… No. Simu …………………. Uhusiano ……………

PICHA YA MZAZI/MLEZI TAJWA

(iii) Jina………………………………...No. Simu……………………...Uhusiano…**……….**...

PICHA YA MZAZI/MLEZI TAJWA

**MEDICAL CERTIFICATE**

DATE …………………

STUDENT'S NAME …………………………………….………………………

(NAME IN FULL)

THE MEDICAL OFFICER:

……………………………………….

………………………………………..

………………………………………..

I have examined the above named student and consider him/her physically and mentally fit for his/her studies. The examination has included the following categories:

a) Eye – sight …………………………………………………….…………...
b) Hearing ……………………………………………………….….………
c) Limbs …………………………………………………………….……….
d) Venereal diseases ……………………………………………...…...
e) Epilepsy ……………………………………………………….…………
f) Leprosy …………………………………………………………...….
g) Neuroses ………………………………………………………………….
h) Other serious Diseases …………………………………………………….
i) Pregnancy …………………………………………………………………

Date ……………………………………………… Signature …………………………
Station ………………………………………….. Designation ………………………